TANGAZO LA SERIKALI NA. 51 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA NSONGWI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Nsongwi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 617 yenye majira-nukta 560925MS, 9013328KZ; baaada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 618 yenye majira-nukta. 561097MS, 9011931KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata korongo umbali wa kilomita 3.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 614B yenye majira-

nukta 561410MS, 9008411KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 3.9 kwa kufuata mpaka na hifadhi ya msitu wa Haporoto hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA612A yenye majira-nukta 558209MS, 9008558 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini Magharibi kwa umbali wa kilomita 3.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 612 yenye majira-nukta 556971MS, 9011155KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji numba VMA 611 yenye majira-nukta 557921MS, 9012917KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki umbali wa kilomita 1.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 613 yenye majira-nukta 559308 MS, 9012592 KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kaskazini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji numba VMA 615 yenye majira-nukta 559720MS, 9012867KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA616 yenye majira-nukta 559659MS, 9013379KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*